

A HUZUNI YA PAULO. Warumi 9:1-3.

❖ Kama Musa, Paulo alikuwa radhi kupoteza wokovu wake ili kuokoa wa Israeli. Kutoka 32:32).

B KUCHAGUA WATEULE. Warumi 9:4-13.

❖ Kwa nini Paulo alikuwa na wasiwasi juu ya watu wa Israeli? Je walikuwa wateule? (Warumi 9:4-5)

— Watu wa Israeli walikuwa wateule kwa sababu walikuwa na upendeleo mkubwa. Mkubwa kabisa Israeli ilikuwa mahali alikozaliwa Masihi: Yesu Kristo.

❖ Kwa nini Mungu alichagua watu wa Israeli?

— Paulo anapozungumzia Isaka na Yakobo, anabainisha kuwa hakuwa na upekee pale Mungu alipowachagua kuwa sehemu ya watu Wake [“kwa maana kabla hawajazaliwa wale watoto, wala hawajatenda neno jema wala baya, ili lisimame kusudi la Mungu la kuchagua, si kwa sababu ya matendo, bali kwa sababu ya nia yake aitaye.” (Warumi 9:11)]. Mungu aliwachagua kwa sababu tu alitaka kufanya hivyo.

❖ Watu wa Israeli walimkataa Masihi, hivyo hawakutimiza utume wao.

❖ Je Mungu alikosea kwa kuwachagua wao?

— Mungu hakosei. Japo uzao wa mwili wa Ibrahimu ulishindwa, utume wao uliendelezwa na uzao wao kulingana na ahadi: Israeli wakiroho (nasi tu sehemu yake)

C KUCHAGUA WATU. Warumi 9:14-18.

❖ Mungu hufanya wengine kuwa na moyo mgumu na kuonyesha wengine rehema. Je; yeye ni mwenye haki?

— Mungu anajua maamuzi ya kila mtu kabla, ili Atangaze hatima yao.

D CHAGUO MAALUMU LA MUNGU. Warumi 9:19-24.

❖ Mungu anamiliki haki ya kuchagua watu fulani kwa ajili ya majukumu maalumu.

❖ Kwa mfano, alichagua wafalme na manabii. Pia anagawa karama za roho namna apendavyo kutoa, sawa na kazi ya kila mshiriki wa kanisa Lake. (1 Wakorintho 12:11).

❖ Mungu amekuchagua wewe kwa jukumu maalumu; labda ni jambo kubwa au ni jambo ambalo dhahiri lina umuhimu mdogo mbele ya watu.

E MUNGU HUMCHAGUA NANI? Warumi 9:25-29.

❖ Israeli walikuwa watu wateule ila walimkataa Mungu. Kisha, Mungu akapanua uteuzi huo kwa wale wasio watu wao: watu wa Mataifa. Uteuzi ulihamishiwa kwa “Israeli wa kiroho.”

❖ Mungu anamasalia maalumu ambao wanapaswa kuifadhi na kuhubiri ukweli.

F MUNGU HUCHAGUA WATU WA AINA GANI KWA AJILI YA WOKOVU? Warumi 9:30-33.

❖ Mungu huwachagua wale wanaokubali kwamba “haki ni kwa imani” ili waokolewe, na kuwakataa wale wanaotafuta haki “kwa matendo.”

❖ “Jiwe” hilo hilo (Yesu) huleta wokovu na hukumu. Luka 20:17-18.

— Wale wanaomkataa Yesu kama Wayahudi walivyofanya “husagwa.”

— Wale waangukao na kuvunjika katika miguu ya Yesu hawataaibika, bali wataokolewa.

❖ Je; moyo wako umevunjwa na upendo wa Yesu? Je, umeamua kuyaacha maisha yako katika mikono yake?